

## HADITHI ZINATAKIKANA!

Je, ulikuwa mpiga kambi, au mtu wa kujitolea, au kiongozi wa rika wakati wowote wa majira ya joto ya mwisho? Una uzoefu wowote ya kufurahisha na wa kuchangamsha, mambo muhimu, mafunzo au mawazo mapya kutoka kwa tukio hilo? Tunataka kusikia kutoka kwako!

Tuambie hadithi yako kwa kutumia SWIS info barua pepe kwa **info@swissask.ca.**

SASKATCHEWAN SWIS COORDINATION
SSC

www.swissask.ca

## WASILIANA NASI KWA TAARIFA ZAIDI:

EAST CENTRAL NEWCOMER WELCOME CENTRE
YORKTON
(306) 783-2777

THE HUMBOLDT REGIONAL NEWCOMER CENTRE
(306) 682-4277

MOOSE JAW MULTICULTURAL COUNCIL
(306) 693-4677

PRINCE ALBERT YWCA
(306) 763-0736

REGINA OPEN DOOR SOCIETY
(306) 352-3500

SASKATOON OPEN DOOR SOCIETY
(306) 653-4464

SOUTHEAST NEWCOMER SERVICES
ESTEVAN
(306) 637-4920

SOUTHWEST NEWCOMER WELCOME CENTRE
SWIFT CURRENT
(306) 778-6262

SASKATCHEWAN SWIS COORDINATION
SSC

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

# UNAJUA CHA KUFANYA WAKATI HUU WA MAJIRA YA JOTO?

Swahili



SASKATCHEWAN SWIS COORDINATION
SSC



## JIHUSISHE!

Ushiriki wako kama mtu wa kujitolea husaidia kuimarisha jamii. Mashirika mengi yanatafuta vijana wa kujiunga na safu zao na kuwapa fursa mbalimbali katika programu zao.

Programu hizi zinaweza kuchangia  kwa maendeleo ya vijana, maisha ya afya na wajibu wa kijamii. Unaposhiriki, unachukua jukumu la kuleta mabadiliko yenye maana, ya kudumu katika ujirani wako, pamoja na pia kupata uzoefu wa Canada, na uwezekano wa kupata marafiki wapya.

## UNASHIRIKI TALANTA ZAKO NA MAARIFA YAKO NA WATU WENGINE.

**Kambi za Mchana wakati wa Majira ya Joto** huwa salama na yenye burudani tele. Kambi hizi hutoa elimu katika nyanja mbalimbali kwa watoto na vijana kwenye kampasi za vyuo vikuu na vyuo vya elimu, huko Saskatchewan.

Makambi haya hutilia mkazo jamii na ushirikiano, na hujitahidi kuwa nafasi ya kuwakaribisha watu wote, jambo ambalo linawatia moyo watu wote kuwa na hamu ya kujifunza chochote katika maisha yao.

Kwa kuzingatia programu ambazo zinazounganisha ‘uzoefu wa maisha’ na zinazoonyesha wapiga kambi uwezekano wa maisha yao ya siku zijazo, jamii tofauti hutoa mchanganyiko wa sanaa. Jamii hizi pia hutoa shughuli za usanii, afya na mazoezi, eco-sayansi, na mtaala wa uongozi kwa kila kikundi cha umri. Vijana hutumia majira ya joto kuchunguza, kujifunza na kupata marafiki katika mazingira ya baada ya masomo ya shule ya upili na mazingira haya hufungua uwezekano nyingi katika maisha yao.

Wapiga kambi wote huwa na umri kati ya miaka 8 na 14 na wana asili tofauti.





## MWONGOZO WA SHUGHULI WAKATI WA MAJIRA YA JOTO

Shule za umma, serikali za jiji na mji, vyuo vya mitaa, mashirika ya jamii, makavazi, nyumba za sanaa, maktaba na mashirika mengine yasiyo ya faida hutoa shughuli mbalimbali za majira ya joto kwa watoto na vijana. (Mara nyingi Wakala wa Makazi huwa na programu maalum kwa vikundi tofauti vya umri.)

Mipango mingi hayatozi **malipo wakati wa majira ya joto.**

**Kuna shughuli jijini Saskatchewan za watoto na vijana wakati wa majira ya joto zenye gharama ya chini.**

**Angalia idara za burudani katika jiji lako au jamii yako.**

## VIJANA NA KAZI YA KUJITOLEA: NI RAHA!!

Watu ambao hujitolea mara nyingi husema ya kuwa wao hufaidika zaidi kutokana na uzoefu wanaopata kuliko kile wanachotoa. Kujitolea kwa kuwapa wengine muda wako na nguvu yako hukufanya uhisi vizuri kujihusu na kuinua heshima yako. Kufanya kazi na watu wengine wa kujitolea hujenga urafiki na watu wengine ambao wana maslahi sawa na huimarisha mitandao ya watu wanaokujua. Baadaye katika maisha, mara nyingi huwa ni ‘unajuana na nani’ ambayo huleta tofauti katika kupata fursa za kazi. Pia, ikiwa umejitolea kwa programu, wakati mwingine unaweza kuelekezwa kupata ajira katika siku zijazo.

Kila mtu ana stadi, talanta, maarifa, tajriba, utu na shauku. Kila mmoja wetu ni tofauti na mwingine na ana kitu cha thamani cha kushiriki na wengine.

